kuwashukuru kwa kututem-

kuelimisha wananchi juu ya

razak Juma.

HABARI LEO UK 15.

# Maofisa ugani wahimizwa kuwa karibu na watafiti, wakulima

Na Mwandishi Maalumu

MAOFISA ugani wametakiwa kubuni mbinu na mifumo itakayowawezesha kuwasiliana kwa karibu na watafiti, wakulima, wafugaji na wavuvi.

Hatua hiyo imeelezwa kwamba itawaweze kuzalisha kwa tija hususani katika kipindi hiki ambapo dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi na maradhi ya corona.

Mwenyekiti wa Chama Cha Wagani Tanzania (TSAEE), Profesa Catherine Msuya alisema hayo wakati akifunga mkutano wa mwaka wa chama hicho jijini Dodoma.

Profesa Msuya alisema kwa sasa kuna mabadiliko ya tabianchi na maradhi ya corona, hivyo lazima waendelee kujikita katika kubuni mifumo na teknolojia zitakazowasaidia kuwawezesha wananchi kuendelea kuzalisha kwa tija na kukabiliana na changamoto hizo.

Ofisa Kilimo kutoka Ilemela, Mwanza, Neema Semwaiko alisema kuwa kupitia mkutano huo wamejifunza mambo mbalimbali mazuri ikiwemo matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) katika kilimo ambazo watakwenda kuzitumia kwenye maeneo yao ya kazi kwa lengo la kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kuzalisha kwa tija.

"Teknolojia hizi tulizopata tunajipanga kwenda kuzitumia kule tulipotoka ili kuboresha mawasiliano kati yetu sisi wagani na wakulima wetu na itatusaidia kuwasiliana na wadau wengi kwa wakati mmoja," alisema

# KANDA YA ZIWA
Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Kagera, Shinyanga

HABARI LEO UK 19

## *Washikiliwa kwa tuhuma za uvuvi haramu

Na Diana Deus, Muleba

KAMATI ya Ulinzi na Usalama, Wilaya ya Muleba Mkoa wa Kagera, inawashikilia wakazi 28 wa Kijiji cha Kyota, Kata ya Kimwani kwa tuhuma za kujihusisha na uvuvi haramu.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya Muleba, Toba Nguvila alisema watuhumiwa hao walikutwa wakitumia makokoro saba na mitumbwi saba.

Nguvila alisema juzi kwamba watuhumiwa hao walikamatwa na wananchi wiki iliyopita, Disemba 2, katika kitongoji cha Kabwinyora, kijiji cha Kihunge, kata ya Rulanda ndani ya Ziwa Victoria.

"Ninafahamu baadhi ya zana hizi ni za matajiri wanaowatuma na bahati nzuri tunawafahamu. Tunaendelea na uchunguzi, tukithibitisha, hata hao matajiri tutawapeleka mahakamani ili iwe fundisho kwa wengine," alisema Nguvila

Alisema wilaya inaendelea kufuatilia mtandao wa watu wanaofadhili uvuvi haramu ili kulinda rasilimali za ziwa Victoria.

Aliwashukuru wananchi waliojitokeza kushiriki kwa hiari katika msako huo, akawataka wakazi wote wa mwambao wa ziwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa namna mbalimbali, ikiwemo kutoa taarifa sahihi ili kudhibiti uvuvi haramu.

Kaimu Afisa Uvuvi Wilaya, Johaiveni Kyaruzi alisema kwa mujibu wa sheria, Kabwiyorwa ni eneo la hifadhi ya mazalia ya samaki ambayo kwa kiasi kikubwa yanaweza kuathiriwa na uvuvi haramu kwani makokoro yanavua hadi samaki wadogo.

"Matokeo yake samaki wataisha kabisa katika Ziwa Victoria," alisema.

Diwani Kata ya Rulanda, Evart Tiletwa alisema wananchi wameshakubaliana kwa hiari yao kuweka doria endelevu ili kukomesha uvuvi haramu.

Hata hivyo, alisema ili kulifanikisha hilo wanahitaji Afisa Uvuvi katika kata yao na vitendea kazi, ikiwemo boti kwa ajili ya doria.

## *Polisi: Wanaum... ukatili wanao...

Na Yohana Shida, Geita

MKUU wa Dawati la Jinsia la Polisi Wilayani Geita, Hidaya Mkariho amesema lipo ongezeko la wanaume wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia na wake zao, hatua inayosabisha migogoro katika familia pamoja na athari za kiafya kwa watendwa.

Mkariho alieleza hayo mwishoni mwa wiki katika mkutano wa kutoa tathmini ya vite... kijinsia, ... shirika ... 'Plan In...

Alis... kua liki... mengi ... wanao...

## Washukuru idadi watoto walemavu kuandikishwa shu...

Na Kareny Masasy, Shinyanga

SHIRIKISHO la vyama vya watu wenye ulemavu (Shivyawata) limepongeza ongezeko la usajili wa watoto wenye ulemavu shuleni, hatua inayohimiza usawa katika jamii.

Hayo yalisemwa na mwenyekiti wa shirikisho hilo, Richard Mpongo, katika kuadhimisha siku ya walemavu duniani ambaye, hata hivyo, alisema bado baadhi ya wazazi hawazijui shule maalumu za kuwapeleka watoto wao.

"Ipo haja ya kuzitangaza shule hizo. Lakini pia bado kuna changamoto ya baadhi ya watoto wenye ulemavu kufichwa ndani," alisema.

Hatua hiyo anasema ililisukuma shirikisho kwa kushirikiana na idara ya elimu mkoa kufanya msako kwa ambao hawajapelekwa shule na kufanikiwa kuwaibua wenye umri wa kuanza darasa la awali, wakaandikishwa.

Alisema wanataka sheria inayosema taasisi kuhakikisha inaajiri asilimia tatu ya wenye ulemavu ifuatwe pia.

"Sasa ili wawepo wenye ujuzi wa kuwawezesha kuajiriwa ni lazima tulazimishe wazazi kuwapeleka shule watoto wenye ulemavu," alisema.

Sambamba na kufaniki-sha watoto kwenda shule, watu wazima (walemavu) pia wamekua wakihimizwa kushiriki shughuli za kiuchumi ambapo wengi wamejiunga na vikundi ili kupata mikopo ya halmashauri kwa ajili mitaji na tayari vikundi 11 vimekopeshwa na kuanza uwekezaji.

Mwenyekiti wa Shivyawata wilayani Kishapu, Josiah Nkinga ambaye pia ni mwalimu wa shule ya sekondari Shinyanga alisema kama ilivyo kwa watoto wengine, wanafunzi wenye ulemavu nao wanafanya vizuri darasani.

Aliiomba serikali kufanya uwekezaji zaidi wa vifaa kulingana na mahitaji ya wenye ulemavu ili kuwawezesha kufaulu zaidi na kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira kama watu wengine.

Mkuu wa wilaya Shinyanga, Jasinta Mboneko aliwataka wazazi kutowaficha watoto wenye ulemavu majumbani, akisema hatua hiyo inawanyima haki ... elimu...



**Baadhi ya waalikwa wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani) alipozungumza katika maadhimisho ya miaka 100 ya Ubuddha Afrika kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam jana.** (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

-RAIA MWEMA UK 6

# Maofisa Ugani wahimizwa ubunifu

**Na Mbaraka Kambona, Dodoma**

MAOFISA ugani nchini wametakiwa kubuni mbinu na mifumo ya kuwasiliana kwa karibu na watafiti, wakulima, wafugaji na wavuvi ili kuzalisha kwa tija hususan kipindi hiki ambacho Dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi na maradhi ya Korona.

Mwito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Chama cha Wagani Tanzania (TSAEE), Profesa Catherine Msuya akifunga mkutano wa mwaka wa chama hicho Dodoma.

Alisema kwa sasa kuna mabadiliko ya tabia nchi na maradhi ya korona hivyo lazima waendelee kujikita katika kubuni mifumo na teknolojia zitakazowasaidia kuwezesha wananchi kuendelea kuzalisha kwa tija na kukabiliana na changamoto hizo.

"Najua tuna mashamba darasa, lakini tuangalie mifumo mingine itakayotukutanisha wadau wote kwa urahisi ili kusaidia wananchi wetu, kwa lengo la kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi," alisema Profesa Msuya.

Naye, Ofisa Kilimo kutoka Ilemela, Mwanza, Neema Semwaiko alisema kuwa kupitia mkutano huo wamejifunza mambo mazuri, yakiwamo matumizi ya Tehama katika kilimo, ambazo watakwenda kuzitumia katika maeneo yao ya kazi, kwa lengo la kuwezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kuzalisha kwa tija. "Teknolojia hizi tulizopata tunajipanga kwenda kuzitumia tulikotoka kwa ajili ya kwenda kuboresha mawasiliano kati yetu sisi wagani na wakulima wetu na itatusaidia kuwasiliana na wadau wengi kwa wakati mmoja," alisema.

Ofisa Ugani kutoka Mkuranga, Julitha Bulali aliiomba Serikali kuendelea kuezesha wataalamu wa ugani wa ngazi zote, ili kuhudumia ipasavyo wananchi katika maeneo wanayofanyia kazi.

"Mkutano huu umetuwezesha kukutana sisi maofisa ugani kutoka maeneo ya nchi na tumejifunza na kubadilishana uzoefu utakaotusaidia kuboresha utendaji kazi zetu," alisema Bulali.

Scanned with CamScanner